

UNAFUMBUA MKONO WAKO

Siku ya Mungu ya 17 Mwaka B

Musique: Charles NYENZE

Texte: Zaburi 144

$\text{♩} = 70$

U - na - fu - mbu - a mko - no wa - ko, ee Bwana na ku - tu - shi - bi - sha.

5

1. Kazi zako zinakutukuza , ee Bwana
na waamini wako wanakusifu
Wanataja utukufu wa ufalme wako,
wanahadisia maajabu ya uwezo wako.

2. Macho ya wote yakutumainia,
nawe unawapa chakula wakati wake.
Wewe wafumbua mkono wako,
wamshibisha kwa ukarimu kila aliye mzima.

3. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,
na mwema katika kazi zake zote.
Bwana ni karibu na wote wanaomwita,
wote wanaomwita kwa uaminifu.